This is a digital copy of a book that was preserved for generations on library shelves before it was carefully scanned by Google as part of a project to make the world's books discoverable online.

It has survived long enough for the copyright to expire and the book to enter the public domain. A public domain book is one that was never subject to copyright or whose legal copyright term has expired. Whether a book is in the public domain may vary country to country. Public domain books are our gateways to the past, representing a wealth of history, culture and knowledge that's often difficult to discover.

Marks, notations and other marginalia present in the original volume will appear in this file - a reminder of this book's long journey from the publisher to a library and finally to you.

Usage guidelines

Google is proud to partner with libraries to digitize public domain materials and make them widely accessible. Public domain books belong to the public and we are merely their custodians. Nevertheless, this work is expensive, so in order to keep providing this resource, we have taken steps to prevent abuse by commercial parties, including placing technical restrictions on automated querying.

We also ask that you:

+ *Make non-commercial use of the files* We designed Google Book Search for use by individuals, and we request that you use these files for personal, non-commercial purposes.

+ *Refrain from automated querying* Do not send automated queries of any sort to Google's system: If you are conducting research on machine translation, optical character recognition or other areas where access to a large amount of text is helpful, please contact us. We encourage the use of public domain materials for these purposes and may be able to help.

+ *Maintain attribution* The Google "watermark" you see on each file is essential for informing people about this project and helping them find additional materials through Google Book Search. Please do not remove it.

+ *Keep it legal* Whatever your use, remember that you are responsible for ensuring that what you are doing is legal. Do not assume that just because we believe a book is in the public domain for users in the United States, that the work is also in the public domain for users in other countries. Whether a book is still in copyright varies from country to country, and we can't offer guidance on whether any specific use of any specific book is allowed. Please do not assume that a book's appearance in Google Book Search means it can be used in any manner anywhere in the world. Copyright infringement liability can be quite severe.

About Google Book Search

Google's mission is to organize the world's information and to make it universally accessible and useful. Google Book Search helps readers discover the world's books while helping authors and publishers reach new audiences. You can search through the full text of this book on the web at `http://books.google.com/`

WIDENER
HN JYIS A
2235
25.106

2235.95.106

Harvard College Library

BOUGHT FROM GIFTS

OF

FRIENDS OF THE LIBRARY

MASOMO MEPESI.

SO
LI
DEO
GL
OR
IA

ZANZIBAR:
1894.
PRINTED AT THE UNIVERSITIES' MISSION PRESS
[EDN. 10, 000.]

2235.95.106
✓

HARVARD COLLEGE LIBRARY
THE GIFT OF
FRIENDS OF THE LIBRARY
Oct 27 1929

N

MASOMO MEPESI.

1.

Kiti chako, kiti chake, kiti cha mtu, kiti cha watu.

Watu wema, watu wale si wema, watu hawa wema sana. Watu gani hawa? Watu wema, watu hawa wote wema.

Watu hawa woga sana. Watu wote woga? Wote woga. Watu wema si woga, watu wabaya woga. Watu hawa wabaya? Wote wabaya sana, siwataki, siwapendi.

II.

Lete kiti, weka kiti hapa. Kiti kipi? Kiti kile kizuri. Kiti kipi kizuri? Kiti hiki kizuri sana. Kiti hiki cha mti, ao cha chuma? Kiti kile cha mti.

Lete kiti cha chuma. Kiti kipi cha chuma? Kiti cho chote kikiwa cha chuma. Kitu hiki cha chuma? Sicho hiki cha chuma.

Nini hiki? Kisu hiki, kisu kile cha chuma kisu, cha mtu huyu cha chuma. Kiti

chake cha mti. Kiti kizuri, kisu kibaya kiti kirefu, kisu kikali, kisu hicho kibaya, sicho kikali.

Shika, peleka, tua, inua, wacha yote pia. Wacheka nini? Nyamaza, nenda upesi, piga mbio, njoo kaa kitako, tulia kimya.

III.

Vaa nguo sasa, vaa nguo hizi. Nguo hizi mbaya. Mbona mbaya? Sijui, mbaya tu, sitaki nguo hizi, nataka zile kule. Nguo gani zile? Nguo mpya, nguo nzuri.

Nguo hizi za taka, sizo nzuri, nataka nguo safi, nguo za mtoto huyu safi sana. Nguo zako si safi, mchafu sana mtoto huyu. Vaa nguo hizi, nguo hizi safi sana, nguo hizi mpya. Shuka hii fupi, siyo nzuri sana. Shuko hiyo si yake, ya nani? Ya mtoto huyu. Bassi mpe, weye vaa nguo zako.

U wapi shuka yako? Si hiyo yake? La, siyo yake, ya mtoto mdogo aliye mfupi sana. Yuko wapi mtoto huyu aliye mfupi? Yuko kule. Mwite, mpe nguo zake.

Vaa nguo hii nzuri. Shuka yake mfupi, lete hapa shuka ile. Mpe huyu shuka hii ya

pili. Hii ndefu? Hii ndefu nzuri sana. Sasa mtoto huyu aliye mfupi ana nguo iliyo ndefu. Nenda zako, usitunze, usitupe tena.

IV.

Baba huyu mkali. Taa hii kubwa. Kazi yake ngumu. Jua kali leo. Dawa yake kali. Mama yako mtu yule. Watu hawa wema.

Dafu lako tamu. Nani huyu? Mtu wako. Fua nasi. Mti huu mkavu. Maji haya haba. Haja zetu kubwa. Papa hapa pema. Nazi kavu zile. Maji ya mvua, maji mema sana. Pana maji hapa. Nipe kisu. Piga kofi. Neno moja tu. Jiwe moja dogo. Watu wema wale. Jina lako nani? Jina langu Ali. Damu yake. Nipe maji ya moto. Jina lake nani? Mali ya watu. Dawa ya watu. Zeze lako. Maji haya ya wapi? Kisa cha Bibi. Kiko chako. Lete chayi. Piga chapa. Lete kuku ile, mpe yule kuku yake.

V.

Pua yako ndefu, pua yake fupi. Tia maji hapa. Baba yake yuko juu. Nina kiu sana leo, lete maji, nipe maji. Paka yake mkubwa, pia yake ndogo.

Meza yako ya mti. Nini hii? Una nini? Mpe maji. Lete unga. Unga gani? Unga wa mchele. Ana choyo sana. Hana choyo mtu huyu, ana chuki.

Lete chuo na chupa la wino. Pana chui kule. Mwenyi mali mtu huyu, ana shamba kubwa sana lenyi miwa. Mtu yule mwenyi mali hajaja.

Hapa pana fisi, na chui, na simba, na nyoka na panya, na mbwa, na mamba, na fungo na tembo, na twiga, na nyati, na nyama wengi tena. Njiwa hawa wema sana. Kazi yangu ngumu sana, sina buddi kuiacha.

VI.

Yuko wapi mama yako? Baba yenu anakwenda wapi? Baba yetu akaenda sokoni. Watu hawa wema sana hawana makelele. Vitu hivi vingi sana, na vitu sita tena viko chini. Kiko hiki chema. Nataka pesa moja. Nipe nyama na wali. Nazi hizi kavu sizo nzuri. Kazi yenu ndogo, fanyeni kazi upesi.

Watu hawa wana choyo. Kusoma ni rahisi, kwa mvivu ni ngumu. Rafiki yako alinipa pesa. Nipe maji somo wee,

Hapa pana fisi. Watoto hawa wema sana. Killa siku soma maneno haya, utajua. Fisi ana woga. Sisi tunayo mali haba tu. Maneno yako mazuri sana, sema neno moja tena. Minazi yako mirefu, yangu mifupi. Wataka nini rafiki? Nataka madafu. Madafu haya makubwa sana, sijui kama matamu. Kijana alikuja jana, akala, akalala, akatoka, akaenda zake. Mtu huyu amesema maneno mabaya. Huyu hodari kuliko mimi, jina lake Uledi, akanipa kisu jana.

Mawe haya marefu. Tazama, watu hawa wanayo maua. Nataka embe, nipe embe zile.

VII.

Haya! Haya! Kazi! Kazi! Yuko wapi fundi Hamisi? Yupo papa hapa, asema ataka chokaa, lete chokaa! Lete chokaa! Sasa lete mawe! Lete mawe! Hapana mawe sasa. Yapo mawe tele. Mawe wapi? Papa hapa karibu yako, si mbali. Huna macho wee? Lete mawe upesi upesi. Sina hatta mawe lete mawe hapa juu, lete! Lete mawe juu. Lete maji tena, hapana maji. Bassi

nenda kateka maji, mwite mtoto Kusi aende ateke maji. Panda juu, ipo ngazi, panda juu. Lete tena chokaa, na mawe, na maji pia.

Yuko wapi mwashi? Mwite. Ewe fundi! kuta hizi mbili bado kwisha? Bado, Bwana, labuda kesho. Kesho? ndiyo kesho? siku zote kesho! Haya, haya! Fanya kazi.

VIII.

Mbwa hali majani, hula nyama tu. Wanapiga mbio wawili wawili. Embe dodo moja pesa. Mtu huyu mretu. Natakupa mchele. Wataka ng'chiro? Lete wali na mchuzi. Mpe mtoto mpila wangu; mpila wako wapi? Sijui.

Mdudu huyu mzuri sana. Mfuko wako mzuri. Mnazi ule mbaya. Mgeni huyu mwema. Mgomba mzuri. Mjakazi wako mbaya. Mbona mbaya? Yule mjanja sana, mpige weye. Mji wake mbali. Mjoli wako mwema.

Mjomba wake atakuja leo. Nataka njugu mawe. Mtu huyu mkali. Lete mkate, kalate mkate wa mofa. Mke wake mwema sana, mke wako mzuri. Mkono wako mfupi.

Mtu huyu mwizi. Si yule mkubwa wako? Fua mkuki. Mkulima huyu analo shamba jema. Mtu huyu ndugu yake, mlevi hana hatta kitu.

Mti huu mnazi, mti ule mwema, mlima ule mkubwa. Usiwe mwivi. Mnara ule mrefu sana. Mnazi mzuri huu. Mti ule mrefu mno. Mbuzi wangu mnono, mbuzi mweusi wako mdogo, kijana bado.

IX.

Nije kesho, Bwana? La! Kesho nina kazi kesho kutwa njoo. Shamba hili mali yangu mimi. Kassi gani embe hizi? Embe mbili pesa moja, embe zile tatu pesa. Embe njema sana. Tangu juzi hatta leo sijala mimi, nipe pesa, kwani sina hatta pesa, nipe pesa moja.

Simba nyama mkali sana, mtu huyu ana hofu. Nguo hizi zangu mimi, ninyi watu wema wenyi haki, nipeni nguo zangu. Mvua nyingi siku hizi; siku hizi za mvua jua kali mno, leo jua kali, jana hapana jua.

Nyanya hizi tamu sana. Kule kwa ng'ambo ya pili kuna watu wengi wenyi mikuki; watu hawa wana mambo mengi. Fua nazi tatu hizi; panda hizi sita, lete hizi mbili mekoni

Ati somo? ya nini una hofu? Cheo hiki sicho cheo changu. Mtu huyu mwenyi chongo Kuna ndege jina lake chosi, anywaye tembo.

Tazama watu hawa, wapiga ngoma, ngoma gani hii? Inaitwa msapata. Mahali pake pabaya sana, pana miiba, na mawe, na shimo.

Tazama chombo hiki kibaya. Nina kazi kucha kutwa. Kazi gani? Usiku nauguza wagonjwa, mchana nasomesha watoto chuoni. Kweli una kazi sana.

X.

Mtu huyu hali kitu. Kwani hali? Sijui, labuda hana njaa. Ana kiu? Mpe maji, bassi sasa ale, mpe maji tena. Maji tele yako. Maji haya si mema, yana taka, nenda 'nje, teka maji mazuri. Maji gani haya? Maji ya mvua. Lete maji ya mvua. mpe mtu yule maji. Si mema maji haya? Mema sana, nipe mimi maji haya, mimi nina kiu. Kwani una kiu wee? Una nini wee? Sema marra ya pili. Nina kiu, nipe maji. Una homa leo? Sema kweli. Sina homa leo, marra ya tatu, nipe maji; sina homa, nina kiu tu. Haya maji, shika kopo, bassi lala sasa. Siwezi kulala,

sina usingizi. Shika kitabu usome, utakuja kweli. Kweli? Kweli. Vema, nitajaribu. Jaribu, utaona.

XI.

Una nini wee? Sema sana, una nini? Una homa? Nina homa leo, nipe uji leo. Uji gani wataka? Uji wa wali mzuri? Nataka uji wa wali.

Uji si huu? Uji huu wa moto sana. Wa moto? Hakuna, si wa moto sana. Haya, sasa kula. Nipe maji, nipe tena kopo la maji, si kopo hili, kopo hili tupu. Kopo baya lile, kopo hili jema, kopo langu miye. Kopo hili silo lako, nipe lako, mimi mtu wako, Bibi, nipe kopo lako la fetha. Liko wapi la fetha? Liko juu. La! Liko 'nje juu ya kiti chako. Haya, lete kopo la fetha. Silo hilo la bati, lako la fetha. Kopo lipi? La fetha. Kopo lako la shaba, silo la fetha. Hili la fetha. Vema, lete. Hili la shaba, mpe mtu yule kwa jikoni hili la fetha weka hapa, juu ya meza.

XII

Mwanangu, kisu hiki cha nani? Chake yeye Bibi. Sicho chake. Kweli, Bibi, chake. Siyo.

Kisu chake cha chuma, kisu hiki cha pua. Kama kisu hiki chema, nipe mimi. Kisu chako si chema, wala si kikali.

Lete visu vitatu vile. Visu hivi vitatu vizuri, tena vikali. Nipe mimi kisu kile, pesa moja ao pesa mia? Pesa mia, Bibi, ndio. Mimi sina pesa mia. Bassi nipe pesa kumi. Pesa hizi pesa kumi? Ziko mia. Bassi sasa kisu hiki cha pua ni chako. Lete kasha lako. Mimi sina kasha. Liko wapi kasha lake? Liko juu ya meza. Haya lete. Sasa wewe lete debe lako. Debe lipi, Bibi? debe la bati, ao debe la shaba? Debe la bati. Liko juu, Bibi, Kasha la nani hili? Kasha la watu wageni wakaja jana. Hakuna, wakaja leo tu. Saa gani? Saa kumi ya jioni.

XIII.

Ali akaja leo, Musa na Almasi wakaja jana. Wako wapi Musa na Almasi? Wako kule chini ya mti. Waite. Mwatoka wapi? Twatoka Bukini.

Lete kiti hapa. Nilete kiti gani? Kiti cha Bibi. Kiti chake sijui kiko wapi. Bassi lete kiti changu. Kiti chako kiko juu? Sasa lete kiti cha pili, nataka viti viwili.

Kwa nini wataka viti viwili ? Nataka kimoja kwa bibi, cha pili nikalie mimi. Bassi, Bibi, taleta kiti cha mama wako kwa bibi, na kiti cha baba wako kwa wee.

Kwa nini waleta kiti kile ? Kiti kile si kizuri. Kiti hiki sicho chako ? Sicho. Bassi, Bibi, taleta chako sasa hivi. Haya, lete, weka hapa chini ya mti; kaa kitako, rafiki, sasa lete habari zako.

XIV.

Mtoto huyu mpenzi wako ? Mpini wa shoka umetoka. Mpera huu mzuri, tuchume mapera, mpishi wake apike mapera haya.

Usitie mrututu. Msafiri huyu hodari sana. Nipe msahafu. Usicheze msapata. Wataka mseto ? Mshahara wake reale mbili.

Nipe mshale, mshale huu wa chuma mkali, sitaki mshale huu. Mshoni yule anashona viatu vizuri vya ngozi.

Msimamizi huyu mkali sana. Msitu wa miti. Msomari mgumu. Piga kinanda, mimi taimba, piga ngoma tucheze. Msukani umevunjika, mashua itapotea. Mtaa wetu ni Mkunazini, wake ni Mbuyuni. Mtu huyu tajiri, huleta mikeka kwa bara huuza. Nipe mtama kwa

punda, punda ana njaa. Mtego mwema huu, mtepe mzuri ule, mto mkubwa huu.

Mtu yule mtoro sana, yule mtumwa wako siye hodari, mvivu yee. Mvua siku hizi nyingi, mvua ya mwaka hii, tulale kivulini. Mwalimu wake mtu mbaya, mwana wake mwizi.

Mtu yule ana mtoto mwana chuoni. Shika mwavuli wangu kwa mkono wa kulia. Mimi mzalia, baba yangu kijana sana, baba yake mzee.

XV.

Mzigo huu mzito muo, mimi mtu mzima nimelemewa. Mbwa wa mwitu yule, kitwa chake kizuri. Mtoto, wee unaitwa na Bibi, ataka kamba mletee. Embe dodo moja pesa, kwenda shamba mbili pesa. Mtende ule mrefu lakini hauzai tende nzuri.

Sitaki halua nataka maandazi ya mchele. Sijui kusema maneno ya kishenzi, najua kizungu miye. Kijana huyu anao upanga wake mkali. Mamba mkubwa sana pale. Kuna mtu aliye hodari kuliko wenzake, mwite amwue mamba yule.

Manyani huiba mahindi, muhogo, nazi na ndizi pia. 'Mbega hula majani, na matunda

ya mwitu. Niletee ndizi nionje, zikiwa tamu ninunue. Vikoi vyetu vibovu kabisa, twataka vingine.

Nataka maji matamu, sitaki madafu. Njoo, tazama punda wangu, mwema ao 'mbaya? Mwite Hamisi, namtaka aje kwangu leo hivi. Mua wako sio mtamu umeoza, lete mwingine.

XVI.

Pana mtu mjini ayari mkuu, ndio kazi yake kuleta watu kwake, husema, Njoo ufanye kazi kwangu, 'takupa reale miteen ujira wako kwa mwezi.

Lakini mwisho wa mwezi humwambia, Nenda mjini kanilie ee vitu viwili, nsipoleta vitu hivi, sikupi fetha yako. Hivyo marra nyingi ayari huyu akapata watu kufanya kazi kwake, pasipo kuwapo ujira wao.

Hatta siku moja akakuta mtoto moja, akaneua naye maneno kama haya, mtoto akajibu, Vema. Akaja kwake akafanya kazi mwezi mzima. Mwezi ukiisha akasema. Nipe fetha yangu.

Lakini bwana wake, huyu ayari, akasema, Nenda sokoni kanilete haa, hii. Mtoto akase-

ma moyoni mwake, Haa, hii ! ndio nini ? Nini haa, hii ? Ah nimejua sasa ! ataona huyu bwana wangu.

Akaenda zake hatta akaona tandu mkubwa, akatwaa chupa nyeusi akamtia mle ndani. Akaenda tena akaona 'nge, na 'nge tena akamtia ndani ya chupa akaiziba. Akaleta chupa ile kwa bwana wake akasema, Nimepata haa, hii.

Bwana wake akasema, Nini hii ? Akamjibu, Tia kidole tu, utaona. Akatia kidole, taandu akamuma, akalia Haa-a-a-a ! Mtoto akasema, Jee ! Bwana umeiona haa, hii pia imo ndani. Bwana wake akajibu, Bassi yatosha. Akampa fetha yake, akaenda zake mtoto.

XVII.

Njia gani hii ? Njia ya Mbweni, Bibi. Njia ya Mbweni ? Haya, twende Mbweni. Mahali pazuri Mbweni ? Ndio pazuri sana, Bibi. Iko nyumba ? Iko, Bibi. Nyumba nzuri, nyumba ya mawe karibu ya pwani. Iko minazi tele, Bibi, na miembe na maua tena, Bibi.

Haya twende Mbweni. Lakini mbali, Bibi. wee huwezi kufika Mbweni. Nathani naweza. Naona mtu kule mwenyi madafu, mwite.

Ewe Baba! ewe mwenyi madafu! ngoja ngoja! kassi gani wakuza madafu? Moja pesa mbili, mawili pesa tatu. Vema, twaa pesa tatu, nipe mawili. Unacho kisu, Butu? Sinacho, Bibi, anacho Maua. Lete kisu, Maua; kata madafu haya, Maua.

Yote mawili, Bibi? Yote mawili, tunywe sote pia. Yuko wapi Milatu? Hajaja? Bado, Bibi. Mwite, tupate kwenda zetu. Milatu! Milatu wee! Njoo upesi, bibi angoja. Twataka kwenda Mbweni, njoo! njoo! Mimi hapa, Bibi. Siswi sote hapa? Haya, twende.

XVIII.

Bwana, wajua nini hii? La, sijui. Ndilo tuta la kupandia viazi. Mboga hizi mboga za viazi? Ndivyo, Bwana, na majani haya huliwa, mpishi wetu hupika mno haya. na viazi vyakula vizuri, vitamu sana. Kule, Bwana, waona muhogo? Majani ya muhogo huliwa? Hakuna, Bwana, machungu, si matamu, na magumu tena, labuda wakati wa njaa majani yake huliwa lakini sijui, sijala mwenyewe. Watu walima mashamba, wapanda muhogo, waiacha miaka mitatu, labuda miaka minne mbele ya kung'oa.

Nini hii, Uledi? Wapi, Bwana? Hii mirefu hii upande wa njia. Ndiyo mtama, lakini mchanga bado, masuke bado kuchanua nikukatie bua moja la mtama? Kata! Ah'sante, refu sana, lapita mrefu wangu. Ndiyo Bwana, lampita mtu mrefu sana likipevuka.

XIX.

Mtoto gani huyu? Sijui. Mtoto mdogo, mzuri sana huyu. Yuko wapi mama wake? Yuko kule. Mwite. Mbaya sana huyu, hataki kuja. Kwa nini hataki kuja? Asema hataki tu, hasemi kwa nini. Mwite tena. Anasema anamfanyia uthia. Hana buddi kuja, mlete.

Mtoto wako yuko hapa; mpe mtoto ndizi hizi. Ndizi hizi mbovu, tamu sana ndizi zile, si njema, ni mbichi. Bassi mpe mtoto ndizi zile zilizo njema.

Nathani ana homa. Mtoto, pika uji, mpe. Hataki uji, asema ataka wali. Wali si mzuri kwa watu wenyi homa, mpe dawa kwanza, kisha mpe maji na uji.

Baba yake kule, Wapi? Kule mtini. Mwite. Mwite tena mama yake, tuwape mtoto wao tupate kwenda zetu nyumbani.

XX.

Nataka mtu kufua chuma hiki. Mwite Musa. Musa hajui sana kufua chuma, kazi yake kufua fetha. Bassi mwite Juma, Juma ndiye fundi sana kwa chuma, kazi yake nzuri sana, hajui kufua fetha, lakini kufua chuma ajua sana, ndiyo kazi yake.

Lete shoka langu. Nataka utie pua, nataka pua njema sana, sitaki chuma. Kweli Bibi, pua ndiyo njema, chuma si vema. Bassi mtu huyu ajua kufua pua, tena yee mtu mwema si ayari, kutia chuma mahali pa pua.

Mpe pesa zake sasa. Pesa ngapi ? Pesa kumi. Naona pesa kumi nyingi. Mpe pesa nane. Hataki pesa nane. Asema kama akitia pua mahali pa kutia chuma sharti umpe pesa kumi. Vema, mpe kumi, bassi nilipate kesho. Vema, Bibi, nitalileta kesho.

XXI.

Nenda sokoni kanunue mafuta. Mafuta gani, Bwana ? mafuta ya uto, ao mafuta ya nazi ? Kwa nini wataka mafuta haya ? Nataka kupaka mlango. Mlango upi ? Sio mlango ule

Mafuta yapi rahisi? mafuta ya uto, ao mafuta ya nazi? Sijui.

Bassi twaa pesa hizi. Kwa pesa kumi hizi nunua mafuta ya uto, na kwa pesa hizi kumi, nunua mafuta ya nazi. Vema, nipe chupa nikatilie. Twaa chupa ile kwa mafuta ya uto, na kikombe hiki kwa mafuta ya nazi.

Nunua kadri ya pesa kumi, ukija nipate kujua mafuta ya uto rahisi, ao mafuta ya nazi. Mafuta ya nazi ghali sana, Bibi. Bassi sina buddi kupata mafuta ya nazi; nataka mafuta ya uto kupaka mlango, na mafuta ya nazi kupaka mkuki wangu. Lete mkuki nipate kuona kama una kutu. Kutu tele, Bwana! Najua, sugua sana. Kiisha paka na mafuta. Mafuta ya nazi? Ndiyo mafuta ya nazi. Vema.

XXII.

Nataka kuza shamba langu. Kassi gani wa kuza? Reale elfu kumi. Ghali sana, siwezi kutoa reale elfu kumi. Lakini, Bwana, shamba langu jema sana, pana maji tele. Pana kisima karibu na nyumba, yamo maji mazuri sana, matamu. Uko tena mto, na maji ya mto mazuri sana lakini maji ya kisima yapita maji ya mto.

Tena katika shamba langu iko miwa tele, na, mtama, na mpunga na maboga zote ziko. Tazama, Bwana, mpunga huu sio mpunga mweusa? Mzito sana. Mpunga huu ndio mpunga wa shamba lako? Kweli Bwana, ndio mpunga wa shamba langu, mimi sisemi uwongo, nasema kweli. Si wakati wa mavuno sasa? Bassi mpunga huo mpunga wa shamba langu.

Minazi mingapi iko shambani mwako? Minazi mia tatu na kenda, Bwana. Shamba lako karibu pwani? Ndio, Bwana, karibu sana pwani, mwendo wa nuss ya saa tu, njoo utazame Bwana.

Liko wapi shamba lako? Si mbali mimi nakwenda katika mashua, kesho, Bwana, saa tatu njoo pwani, twende sote. Kufika lini? Labuda muda wa saa ya 'nne. Jua kali sasa, siwezi kwenda saa ya, nne. Bassi, Bwana twende saa ya, kwanza tufike saa ya pili. Vema kesho saa ya kwanza twende.

XXIII.

Wataka mua? Nataka. Bassi twaa mua

mmoja wa katika miwa hii. Ahsante. Wauona mtamu ? Mtamu sana, Bwana, lakini mua wangu si mtamu. Kwa nini si mtamu ? Sijui, labuda mkavu. Nathani mkavu. Siku hizi hapana mvua, sababu hii miwa mikavu yote. Lete mua wa pili nipate kuonja. Huu mtamu ati, kipande kidogo mpe Bibi. Bibi hataki mua. Siyo, yee hula mua. Vema, tukate. Menya kwanza, kiisha kata vipande vidogo vidogo, hataki vipande vikubwa kama vyetu. Kiisha mpe Bibi.

Sasa lete sahani nitie. Sahani ipi ? Sahani ile, sahani ndogo. Hizi zote ndogo hizi zote sawa sawa. Vema, lete sahani mbili. Tia mua. Sasa, chukua ! Yuko wapi Bibi ? Hako chini ? Hako. Labuda yuko juu chumbani mwake. Niende juu ? Nenda peleka.

XXIV.

Hodi ! Hodi ! Karibu, Bwana, karibu, kaa kitako, kaa kitako. Nimekaa, jambo, Bwana, jambo. Hujambo ? Sijambo. Habari gani ? Njema. Za siku nyingi ? Njema. Kwa nini sasa huji, Bwana ? Siku nyingi sasa hukuja. Ah ! tangu siku nyingi siwezi. Hu-

wezi nini? Homa? Kitwa. Wataka dawa? Nataka. Twaa dawa hii. Dawa gani hii? Dawa ya kitwa. Tia maji, kiisha kunywa. Yote, Bwana? Yote pia, jua likichwa mbele ya kulala.

Nataka dawa ya usingizi, Bwana, usiku silali. Bassi twaa dawa hiyo, siwezi kukupa dawa ngine, dawa hiyo njema sana, lakini chungu. Kali, Bwana? Si kali chungu tu. Kunywa upesi yote pia, kiisha kunywa maji. Maji baridi, ao maji ya moto? Maji ya baridi afathali.

XXV.

Naona mapera mtini. Ndio, Bibi, yako, lakini si tayari bado, mabichi tu. Lete moja nipate kuona. Tazama, Bibi, bichi tu, rangi yake kama majani. Ati Hamadi, tazama tena, kama liko moja bivu. Liko wapi, Bibi? Liko juu kabisa.

Ah! siwezi kulichuma mimi, sifiki. Jaribu! panda juu. Hatari nyingi, Bibi, siwezi. Fanya juhudi, nataka pera lile-lile kwa sababu kuwa bivu. Haya Bibi! nitapanda.

Mabruki! Mabruki wee, lete fito. Fito gani, Bibi? Fito ile ndefu. Niletee pera hili-

Ee Bibi, pokea pera lile. Tamu? Tamu sana. Kesho kutwa tuchume mengine, ikinya mvua. Kweli, ikinya mvua; lakini sasa mawingu hapana, jua kali sana, hatta mvua hapana mpaka siku kumi labuda. Labuda, kua heri, Bibi. Kua heri.

XXVI.

Bibi, saa a sita sasa. Kweli saa a sita, lakini maana yake kusema saa a sita? Wakati gani saa a sita? Saa a sita, Bibi, wakati wa kula. Bassi chakula si tayari? Tayari, lakini bado kusali. Vema! nyinyi tayari? Killa mtu kwa mahali pake? Tayari, Bibi!

Chakula gani leo? Chakula kizuri sana, wali na mchuzi. Bibi, hapana maji! Juma! Twaa ndoo ndogo ile, si kubwa, kateka maji. Kuteka wapi, bibi? Katika birika. Birika liko chini ya kanisa, maji yale mazuri sana. Ndiyo Bibi. Birika la maji ya mvua. Kula kwanza, kiisha nenda kateka maji tena. Vema, Bibi!

XXVII.

Tazama, Bibi! Chui yuko kule, chini ya mti. Kweli chui hatta mimi, namwona lakini

si wazi. Usiku huu alikuja chui akala kuku wawili. Nathani siyo chui, ni nyoka chui hawezi kuingia nyumbani kwa kuku, lakini nyoka hupenya katika tundu dogo sana. Nathani nyoka alikula kuku. Kwetu siku ile nyoka alikula kuku kumi na tatu, na mayayi tele ! Lakini sasa kule kweli naona ndiye chui. Mimi sioni kitu. Yuko kweli, Baba, tazama sana, chini ya mti ule mkubwa, 'mbuyu ule, chui yuko katika magugu, waona macho yake ? Kweli namwona sasa, lete bunduki yangu. Risasi hapana, Baba, wala hapana baruti. Risasi ziko kashani mwangu, na baruti pia ndani ya pemde. Iko wapi pembe, Baba ? Tokea siku ya Jumaa sikuona pembe lako wala langu. Ziko juu zote mbili, zimetundikwa juu ya paa.

Ati Baba ! Waonaje shauri langu tuchimbe shimo, tutege mtego. Naona shauri lako ndilo shauri jema, kesho tuchimbe shimo, chui akifa shimoni tutwae ngozi yake tuuze. Kwa nani ? Labuda kwa Magoa ao Wazungu tutalipwa kuku zetu, na kucha zake nzuri tena, watu wengi hupenda kununua kucha za chui ao kucha za simba

XXVIII.

Mambo, njoo, lete hapa chupa yako. Iko wapi chupa yangu ? Iko pale juu pa meza ile. Chupa hii si chupa yangu ; chupa yangu kubwa, chupa ile ndogo sana. Kama chupa hii si chupa yako, ndio chupa ya nani ? Chupa ya mtoto mgeni labuda. Mtoto yupi mgeni ? Jina lake nani ? Jina lake Shame, Bwana. Bassi mwite Shame. Shame ! Njoo ! Njoo ! Naja, Bwana. Shame chupa hii ndiyo yako ? Ndiyo, Bwana. Na chupa hii ya pili, ndiyo ya nani ? Chupa ipi ? Chupa hii nzuri ? Ndiyo yako, Bwana. Siyo chupa yangu ndefu mno, chupa hiyo fupi. Chupa yangu iko juu, siyo hapa. Sema, Mambo, hiyo ndiyo chupa ya nani ? Sijui, labda chupa hii siyo mali ya mtu, chupa tupu ya wino tu. Vema, lete chupa yako, chupa yako safi, sasa weke hapa juu ya meza, haya lete asali ile nitilie.

XXIX.

Njoo, Kisa, lete kuni, lete tena mawe, fanya jiko, lete chungu kile, sasa koka moto, twaa mchele huu, tia ndani ya chungu, tia maji, pika wali mzuri kwa wewe, na

Maua, ua Msimu, ua mimi, tule sote. Zi wapi nazi, Bibi? Nipe nazi mbili. La! Twaa nazi moja tu, lete mbuzi kazikuna; pika mchuzi mzuri.

Chinja kuku mmoja, chinja kuku moja leo, na kuku ya pili kesho. Nipe chumvi, Bibi. Sina chumvi hapa, iko chumvi tele ndani ya kasha kubwa la chuma. Nenda juu, twaa chumvi kwa mchuzi, twaa pili-pili tena na ndimu fanya mchuzi mzuri.

XXX

Bwana, mwenyi maziwa ataka fetha yake. Mimi simpi fetha yake leo, mwambie kesho kutwa ndiyo siku ya kupata fetha yake, akija kesho kutwa saa ya tatu 'tampa fetha yake.

Asema, Bwana ataka umpe fetha yake leo hivi kwa sababu mtoto wake hawezi, ana homa, hawezi sana ataka kukopa fetha yake anunue mchele afanye uji kwa mtoto wake.

Vema lete kasha langu la fetha, sina buddi kumpa fetha huyo akitaka kwa mtoto mwenyi homa, mpe tena dawa, kwa mtoto wake. Wajua kama mtoto huyu mdogo ao mkubwa? Sijui, Bwana, ana watoto wawili, mmoja mdogo

mmoja mkubwa, labda mdogo aliye hawezi leo.

Bassi mpe fetha yake kassi gani ? Asemaje ? Asema, Bwana, ataka reale kumi leo, na reale tano kesho kutwa. Kesho kutwa ndiyo siku ya tano ya mwezi, siku yake. Ndiyo siku yake lakini si siku ya tano, ndio siku ya nne ya mwezi, leo siku ya pili kesho siku ya tatu, kesho kutwa siku ya nne, ndio siku ya kupata fetha yake. Akija kesho kutwa atapata reale tano hizi ? Atapata, aje kesho kutwa bass !

XXXI.

Yuko wapi yule mtoto mdogo sana ? Huyu mtoto mdogo. Kweli huyu mdogo, akaja lini ? akaja jana. Hakuja leo ? Hakuna, akaja jana usiku. Usiku saa ngapi ? akaja saa ya pili usiku giza sana. Yuko wapi baba wake ? Sijui.

Je ! mtoto, njoo hapa. Jambo ? Sijambo. Yuko wapi baba wako ? Sijui yuko wapi. Katika mji ama katika shamba ? Sijui, baba yangu kenda zake. Kenda zake wapi ? Kenda zake sokoni kenda sokoni kuza kuku. Kuku ngapi anazo

Sijui, labuda kumi. Kumi wengi sana, kuku hizi kumi zote zake? Hakuna, za bwana wake, moja yake tu. Bassi jumla kumi, ama kumi na moja, Jumla kumi na moja, moja yake, kumi za bwana wake. Bassi yuko wapi sasa baba yako? Sijui. labuda yuko sokoni.

Wataka kuketi hapa? Nataka hapa, hapa pazuri sana, pana raha na kushiba. Lakini mtoto gani wee? Raha gani pasipo baba wako, na mama wako? Mama yangu amekufa, baba yangu sijui yuko wapi, nataka kuketi hapa kusoma. Kusoma! Kweli kusoma. Kukaa hapa kula labuda? Kusoma na kula ni raha, hapa kusoma na kula. Nataka kusoma na kula, na kucheza bassi. Haya nenda kwa watoto wenzako chini. Ahsante, Bwana.

XXXII.

Bibi, mbuzi yuko huko, anakula majani, anakula mua wetu, mbuzi huyu mbaya sana, anakula yote; sasa tazama anakula muhogo-muhogo wa Mabruki, sasa tazama tena anakula viazi sasa; viazi vyako, Mtoka, anakula vyote. Killa siku huja mbuzi huyu kula majani, na miwa na muhogo, na viazi, na vitu

vyetu vyote pia, ndiyo kazi yake.

Killa siku anakuja, akaja jana, akaja juzi, akaja usiku wa leo tena, mchana na usiku, killa siku killa siku anakuja anakula, anakula, vyote pia anakula, jana akala mchicha, leo akala muhogo, juzi akala miwa na nyanya. Na maua tena anakula, anakula maua yako, Bibi, hapana maua tena amekula yote pia, hatta njugu akala. Haya watoto, nenda mkamateni! wee Shame nenda, nenda, Mabruki, mkamateni, wee tena Mtoka, nenda, Mtaiwa, nenda. Bibi, sisi sote twende? Hakuna, wasiende watoto wadogo, wakubwa waende tu.

Haya njoo, Mabruki, huyo! huyo! yuko kule, haya! haya! mbio jamaa! Shame mbio! Yuko wapi sasa? Yuko nyuma ya muhogo. Haya tazama, Mtaiwa, karibu yako mkamate!

Mshike sana, tazama, Bibi, yupo hapa. Wapi kamba? Lete kamba, kamba hii fupi, lete kamba ngine, kamba ndefu, kamba nzuri. Twaa kamba hii, kamba mpya hii, ndefu tena. Mfunge sana, mfunge hapa nyuma ya nyumba, sasa mpe maji, labuda ana kiu, mpe tena majani, ana njaa. Bibi, tokea hapo

amekaa hapa kula majani na miwa yetu, ameshiba sasa kweli hana njaa.

Yuko wapi mwenyi mbuzi huyu? Sijui. Wajua wee, Mabruki? Najua anakaa kule katika nyumba ya mawe ile kubwa sana, anao mbuzi wengi sana, wangine wadogo, wangine wakubwa, wangine weusi, wangine weupe, wanakuja hapa wote, wanakula sana hapa, killa siku wanakaja, Bassi nenda kamwite aje amkomboe mbuzi wake.

XXXIII.

Bwana, njoo tazama kima huyu, mwenyewe anakuza, kima mzuri kijana tu bado, si mzee. Kima huyu mwema sana, haumi kabisa, mwenyewe asema sasa hataki kuza. Kwa nini hataki kuza? Sijui, hataki tu. Mwite. Anakuja, na kima yake. Tazama kima anakaa begani mwake, sasa anashuka. Jee Almasi, mwoga wee! ginsi gani kuogopa? haumi. Ana meno, meno yake makali sana. Lakini haumi ati! Je Baba, wataka kuza? Sijui, Bwana.

Kassi gani wakuza? Reale mbili, Bwana. Reale mbili! Bassi nenda zako, ghali sana, sitoi reale mbili kwa kima, kima hana fayida,

fayida gani kutoa reale mbili kununua kima? hafanyi kazi, wala haseme, hana neno, hana nguvu, wala si mzuri, kazi yake kula tu. Bassi Bwana, asema, kassi gani? Nitakupa robo. Robo, Bwana, siwezi, siuzi kima wangu kwa robo reale, Bwana, twaa kwa reale. La! nussu reale labuda. Sema kassa robo, Bwana Sikupi, nussu reale tu tatoa.

XXXIV.

Almasi njoo hapa, mbona unavaa nguo hizi za taka? Haifai kuvua nguo za taka. Sina ngine, Bwana nguo zote zina taka. Bass, njoo fua nguo zote upate nguo safi, nzuri, Vema, nipe sabuni bassi. Sabuni ni hii, haya twaa. Sabuni hii, kidogo, Bwana, haitoshi. Mimi nathani yatosha, fua bass, tuone.

Nenda sasa kateke maji, lete maji hapa na sabuni, na nguo zako zote, nataka ufue nguo zako zote pia. Nitavaa nini, Bwana? Twaa kaniki hii, kavae. Sasa nguo zako zote zipo hapa? Zipo hapa, Bwana. Haya hesabu, Mosi, pili tatu, 'nne, tano, sita, saba, nane, kenda, kumi, kumi, na moja, kumi na mbili, Bwana. Nguo zako nyingi sana, mtoto mdogo kama wewe unazo nguo kumi

Bassi na mfuko uko wapi? Uko juu. Lete mfuko, kafua mfuko pamoja na nguo zako Mfuko safi sana, Bwana. Lakini lete mfuko nitazame. Mfuko huu si wako. Mfuko huu mfuko wa Mabruki. Tazama hii! si jina lake Mabruki? Uko wapi mfuko wako? Sijui, Bwana. Nenda juu kalete mfuko wako wewe, chukua huu mpe Mabruki, hakosi Mabruki ametwaa mfuko wako. Mwite Mabruki, mpe mfuko wake yeye, kasema, wataka mfuko wako, labuda utapewa. Bwana, Mabruki asema, hana mfuko wangu, mfuko ulio juu ndio wake. Mwambie amekosa bassi. Mfuko wake si huu? Mwite aje upesi, alete mfuko ulio juu karibu na wake tupate kuona, tutambue wako na wake. Haya upesi, Mabruki. Ameleta mfuko, Bwana, lakini mfuko huu si wake, ndio wangu mimi. Kweli hili ndilo jina lako Almasi, hili ndilo jina lake Mabruki. Sasa killa mtu atwae mfuko wake. Tunza sana. Ukipotea, utapata kupigwa sana.

XXXV.

Bibi, yuko mtu chini, anakuza kuku. Kassi gani moja? Sijui, Bibi. Mwite bassi. Huyu, Bibi, anakuza kuku; miye nataka kuku, Bibi,

kuku moja. Je Baba, kassi gani kuku huyu? Moja robo, Bibi. Ghali sana, mtoto huyu hana mapesa mengi, hawezi kutoa robo, mpe kuku moja kwa pesa kumi na tano. Kumi na tano siwezi, Bibi, kumi na nane labuda. Hana mapesa kumi na nane. Mapesa yake kumi na sita tu, hana mengine, na yee anataka kuku kwa pesa kumi na tano, hataki kutoa pesa zake zote, mpe bassi kuku huyu kwa pesa kumi na tano. Huyu mkubwa, Bibi, siwezi, kumpa kwa pesa kumi na tano. Haya tazama, Bibi, huyu mdogo sana, nipe huyu bassi. Pesa kumi na sita, Bibi; kuku sasa ghali sana, huko Mlima kuku rahisi, huuzwa huko tatu kwa robo, 'nne kwa robo, lakini siku hizi kuku hamna mjini, watu wengi wako mjini, wote hununua kuku, sokoni hapana. Nimetoka shamba leo, nimeleta kuku hizi, sababu Bwana akasema, sharti nilete reale mbili kwa zile kuku saba. Haya kua heri, Bibi, nimekuza kuku rahisi sana. Ah! mwenyi kuza husema rahisi, mwenyi kununua husema ghali. Kweli, kweli, hii desturi ya watu, Bibi.

XXXVI.

Mwite Daudi. Daudi, nataka mchele kwa

watoto. Mchele rahisi sasa? Sijui, Bibi, uko pishi tatu kwa reale, uko pishi tano kwa reale uko tena pishi tano u nusu, uko tena pishi sita kwa reale, na pishi saba, hatta pishi nane kwa reale, lakini huu mbaya, si mzuri. Mimi sitaki mbaya, nataka mzuri, lete mchele pishi sita kwa reale; twaa reale tatu kwa mchele, tena nataka muhogo. Muhogo mbichi ama mkavu? Muhogo mkavu kufanya ugali. Kassi gani muhogo sasa? Pesa kumi na sita Bibi, kwa kikapo kimoja, Vema, haya mapesa kumi na sita, na pesa kumi kumpa mwenyi kutwanga. Bibi, hataki kumi kutwanga kikapo kimoja, asema ataka pesa kumi na sita. Vema, mpe kumi na sita; tena nataka kunde, pishi ngapi kwa reale? Labuda pishi kumi, kunde rahisi sana.

Vema nunua pishi kumi. Twaa reale hizi tatu kwa mchele, na robo tena kwa kunde, kwa kikapo kimoja cha muhogo pesa kumi na sita na mwenyi kutwanga pesa kumi na sita, robo jumla. Kweli, Bibi, jumla ndio robo. Bassi sasa lete yote pia, mchele, na muhogo, na kunde. Ndio Bibi, najua, kunde na muhogo na mchele. Haya usikawie, watoto hawana chakula leo

XXXVII.

Njoo, Hamisi twaa mapesa haya, nenda sokoni, nataka miwa ; nunua mizuri kwa pesa kumi na sita, tena nunua ndizi, ndizi nzuri, ndizi kisukari ; pesa tano kwa ndizi, siku hizi ndizi ngapi pesa ? Sijui, Bibi, labuda tano kwa pesa. Vema, pesa tano zatosha kwa ndizi, tena nunua embe, embe kubwa, embe nzuri. Embe dodo, Bibi ? Ndio embe dodo. Embe dodo moja pesa, moja pesa mbili. Vema, embe dodo pesa kumi na mbili, embe dodo nzuri sana moja pesa mbili, embe sita, waona ? Najua, Bibi. Tena nataka embe mbichi. Siku hizi, Bibi, embe mbichi hapana, shidda. Hatta embe dodo mbichi hapana ? Labuda, Bibi, embe dodo mbichi. Vema embe mbichi kwa pesa sita, tena nunua viazi, viazi vizuri. Pesa ngapi, Bibi ? Pesa mbili kwa viazi, viazi rahisi sasa. Tena kiazi kikuu kimoja kwa pesa tatu labuda utaona, chagua kizuri, hatta kikiwa pesa nane nataka kizuri. Tena nataka mbaazi, mbaazi mbichi, mbaazi si ghali sasa ? Hakuna, Bibi, rahisi, fungu moja kwa pesa, fungu moja latosha wa mtu moja. Bassi kwa watu wanne, ma-

fungu manne, Haya twaa pesa nne kwa mbaazi, wajua sasa ? Miwa, na ndizi, na embe dodo, na embe mbichi, na viazi, na kiazi kikuu, na tena mbaazi, bassi haya nenda upesi.

XXXVIII.

Watoto, nataka maua, leteni maua mazuri. Maua gani, Bibi? Maua haya waona, haya karibu hapa, chuma yale juu, juu sana siwezi mimi kuchuma yale yaliyo juu, lakini panda juu wee, Chivoko kachuma, chuma mengi, haya mazuri sana. Vema, sasa nataka maua meupe, nataka mengi, tena nataka majani, majani mazuri. Kama haya, Bibi? Kama haya, yatosha, lete mengi.

Bibi, tazama maua haya makubwa mazuri Ndiyo makubwa, yako mengi? Hakuna yako mawili tu kama haya, lakini haya madogo mazuri. Loo! Bibi haya mazuri! nusa, Bibi! yanuka vizuri sana. Njoo hapa afu tele, afu tele! Haya chuma, chuma virefu, nitie ndani ya maji. Haya vifupi, Bibi. Siyo, vizuri, virefu sana. Tazama mtoto huyu, Bibi, akachuma vizuri virefu. Mimi mona maua yaliyo mazuri ni afu, yapita yote, sababu ya kunuka vizuri.

XXXIX.

Bibi, mtoto huyu ajua kusoma, ajua A, B, CH, ajua zote mpaka Z! Kweli, Bibi, mpaka Z ajua. Haya, mtoto, njoo soma, nini hii? O. Na hii? P. Na hii? CH. Na hii? L. Na hii? R. Vema! Sasa hii tena? NG'. Na hii? M. Vema. Wajua zote pia? Ajua zote pia, Bibi, tokea jana amejua, ana akili sana huyu. Mdogo, lakini ajua kusoma kupita wenzake sababu wenzake wote wavivu sana, huyu killa siku anasoma sana, anasoma, anasoma, wala hachoki. Wale wakisoma killa siku wasema wamechoka, wamechoka, bassi sasa huyu mkubwa mvivu sana, hatta leo hivi hajui kusoma, uvivu tu! anazo akili lakini mvivu tu. Huyu mdogo hachoki, killa siku anasoma hachoki, sasa anajua upesi, kesho ataanza, "Masomo Mepesi,' hatta mwisho wa mwezi huyu atasoma " Maandiko Matakatifu."

XL.

Bibi, komba hana chakula, ana njaa. Vema, mpe chakula hiki cha wali, kidogo tu, tena twaa ndizi hizi. Ndizi hizi mbovu. La

si mbovu, zote nzuri, zatosha kwa komba hizi nzuri sana, nazitaka kwa watoto kesho. kesho watoto hupewa ndizi, kesho juma a pili, bassi hizi zatosha kwa komba, mpe hizi. Ndizi zile zilizo juu ya meza uache, usitwae zile, twaa hizi zilizo chini karibu ya meza, zile zilizo juu ya meza nataka kwa Bwana mkubwa zilizo chini zafaa kwa komba, tena twaa wali huu, komba apenda sana wali. Apenda wali wa mtama, ama wali wa mchele? Apenda zote mbili, lakini apenda wali wa mchele kuliko wali wa mtama. Na wee tena waona upi mtamu, wali wa mchele ama wali wa matama? Naona wali wa mchele mtamu kupita wali wa mtama. Mjinga wee! kweli wali wa mchele mtamu lakini hauna nguvu, wali wa mtama una nguvu sana.

XLI.

Labuda kima ya Bwana ana kiu. Labuda, mpe maji bassi. Hapana maji, Bibi. Mbona hapana maji? Sijui wapi ndoo. Hii hapa, lakini maji hamna. Hamna hatta kidogo? Kidogo yatosha kwa kima. Hataki maji mengi. Maji kidogo tu yatosha. Hatta kidogo,

Bibi, hamna. Lete ndoo hapa. Mwite Almasi ateke maji. Almasi! Almasi wee! Njoo! Bibi ataka maji. Maji ya birika? Ndio maji ya baridi. Maji yako kule ndani pipa, maji mazuri sana, maji ya mvua. Lete bassi maji haya. Sasa mtoto, twaa kopo hili la bati kampe kima maji. Li wapi kopo? Sioni kopo. Kopo si hilo karibu yako hapa juu ya kiti chako? Haya! haya mtekee maji, bassi. Nimempa. Bassi nenda zako kucheza chini. Lakini wambie wangine wasifanye makelele sana. Vema, Bibi.

MBWA.

Kuko huko Ulaya mbwa hupendwa sana hutunzwa sana, tena huuzwa ghali.

Kuna namna nyingi za mbwa huko Ulaya, hatta ungesema si nyama moja kwa maana umbo wao mbali sana.

Wangine wana nyele ndefu sana tena nzito hatta kupita mbuzi, wangine nyele zao laini kama hariri; wangine wakubwa, wanene; wangine warefu lakini wembamba, wao huenda mbio sana. Wangine tena wadogo sana kama kadri ya buku. Wao wadogo hupendwa

nyumbani, bibi za Wazungu huwapakata, huwabembereza.

Na mbwa hao wana akili sana. Wamefundishwa mambo mengi. Mtu akienda kupiga ndege shuti afuatane na mbwa. Mbwa huyu akisikia harufu ya ndege ya namna apendayo bwana wake, mbwa atasimama kimya, hamrushi ndege hatta akija bwana wake karibu apate kumpiga. Tena ndege akipigwa, akianguka, huyu mbwa atamtafuta hatta amone amletee bwana wake. Atamshika kwa mido domo atamletea asimtafune hatta kidogo.

Kuna tena mbwa, bwana wao kikimpotea kitu njiani atamwambia mbwa, Nenda katafute. Mbwa atarudi kutafuta kunusa-nusa njiani hatta atakuta mali ya bwana wake. Ataijua kwa kusikia harufu ya bwana wake, atashika, atai mletea bwana.

Palikuwa na mbwa mmoja mkubwa na mzuri sana. Alikuwa hodari sana kutafuta vitu na kuvichukua. Siku moja bibi yake alikuwa akimsomea mtu masikini mgonjwa, orofani juu. Mbwa alikuwa alikaa nje, maana akakatazwa kuingia nyumbani, na yeye husikia, kukaa pale pale nje.

Bassi bibi akiisha kusoma, akaondoka akamwaga yule kizee mgonjwa, akaenda zake yule bibi.

Bibi akasahau mwavuli wake huko huko kwenyi kizee, hatta akafika nusu ya njia kurudi nyumbani mwake, akaona kumbe ! hapana mwavuli !

Bibi huyu hataki kurudi amechoka, bassi akamwita yule mbwa akamwambia, " Haya nenda katafute."

Mbwa akamtazama bibi marra moja, kiisha akaenda zake mbio, akinusa huko na huko akitafuta kimpoteacho bibi yake.

Naye mbwa hana habari kama ndio mwavuli ama kitambaa chake, ama chuo chake, ama nini akatafuta tu.

Akaenda, akaenda, akaenda hatta akafika kule kule nyumbani kwa kizee. Akaingia nyumbani akawa akitafuta mali ya bibi yake.

Kwanza hathubutu kuingia nyumbani, sasa akaingia, maana akatumwa na bibi yake.

Akapanda daraja hatta kwa chumba cha mgonjwa. Huyu akasangaa akimwona mbwa mkubwa yule. Lakini marra mbwa akaona mwavuli wa bibi yake, akaja akaukamata

mdomoni akashuka zile daraja akamfuata bibi yake mbio mbio hatta akafika pale alipokuwa bibi, akampelekea mwavuli wake.

Bibi akafurahiwa sana akambembereza mbwa, akamwambia, "Mbwa mwema wee!" hatta mbwa akachapachapa na mkia akifurahi sana.

Hapa Unguja ndio desturi ya watu wakimwona mbwa humpigia mawe, husema, "Huyo! huyo!" hatta mbwa hukimbia huko na huko wala hajui atokako wala aendako.

Mbwa huyu amekosa nini watu wampige hivyo? Anapigwa burre masikini, hakukosa anatembea tu. Bassi vibaya kupiga nyama yo yote burre. Akiwa mbwa wako amekosa, mpige, umrudi, lakini kupiga mbwa burre sababu anatembea tu, si vema.

Mbwa hawa wa Unguja hawana akili kama mbwa wa kizungu, wala hawakufundishwa, wanaonewa, wanafukuzwa tu.

Lakini hatta mbwa hawa wanatufaa sisi waana Adamu.

Sikia, punda akifa, ama ngamia, mzoga wake hutupwa pwani. Ungekaa pale pale, ungenuka vibaya, ungetuthuru hatta wengi watapatwa

na ugonjwa sababu ya uvundu wake.

Lakini killa siku huja mbwa wengi hula nyama hii hatta imekwisha, imesalia mifupa mitupu isiyoliwa. Bassi kazi njema hii ya mbwa; wanatufaa sisi, haifai kuwapiga.

KISA CHA NGAMIA NA MASIKINI.

Palikuwa na masikini, alikaa peke yake mwituni, killa siku hutoka kwenda njiani kuomba tu, ndiyo kazi yake.

Siku moja akakutana na watu waliotafuta ngamia yao aliyepotea.

Wakamwambia, "Ewe baba, ngamia wetu amepotea, umemwona?"

Akawaambia, "Ngamia wenu mwenyi chongo, ama siyo?"

Wakamwambia,"Kweli mwenyi chongo umemwona wapi bassi?"

Akawaambia, "Tena ngamia huyu kiwete, mguu wake wa kushoto unamuma?"

Wakamwambia, "Kweli, baba, bassi yuko wapi?"

Akawaambia "Ana pengo huyu ngamia?"

Wakamwambia, "Kweli kweli, baba, utuambie umemwona wapi?"

Akawaambia, "Tena naona mzigo wake upande wa kulia ndio mpunga, na upande wa kushoto amechukua asali."

Wakamwambia, "Umejuaje mizigo yake? lakini kweli maneno yako, umemkuta wapi bassi?

Akawaambia, "Bassi ngamia huyu sikumwona, hatta marra ya kwanza sikumwona."

Wao wakakasirika sana, wakasema, "Ee mzee wee! mwongo wee! Umemwona, umetuambia habari zake zote, ginsi ana chongo ana pengo yu kiwete, hatta mizigo yake umetuambia bassi mbona hukumwona? Mwongo wee."

Huyu masikini akajibu tena, akawaambia, "Nawaambia kweli ninyi, sikumwona ngamia wenu."

Bassi wakamchuka kwa kathi, wakamshitaki wakasema, "Huyu amemwona ngamia wetu aliyetupotea, ametuambia habari zake zote, hatta mizigo yake, lakini kusema yuko wapi ngamia wetu anakataa."

Yule kathi akaamuru apigwe. Wakamfunga, wakataka kumpiga, yeye akasema, "Sikia Bwana! na ngamia wao sikumwona lakini nali-

pokuwa nikitembea nikaona nyayo zake za ngamia mchangani, naliona tena ana chongo, maana anatafuna majani kwa upande mmoja tu wa njia, haoni yaliyoko mazuri zayidi kwa upande wa pili; tena nikaona ana pengo sababu killa anapotafuna majani, yanabaki vichache vizima katikati; tena kiwete, kwa maana uyayo wa mguu mmoja hankuandikwa vema, nikaona hawezi huyu kukanyaga sana na mguu mmoja."

Wao wakastajabu, wakamwambia, "Mizigo umepataje kuitambua usipoiona?"

Akawaambia, "Ndege wakifuata nyayo zake kwa upande mmoja wakanicnyesha kama alichukua mpunga kwa upande huu, tena mamzi wakarukaruka kwa upande wa pili wakanionyesha kama amechukua asali kwa upande huu. Haya yote nimetambua kwa kutazama na kufuata nyayo zake za ngamia, tena nawapasha habari nga ni huyu amepotea wala hakuibiwa maana hapana nyayo za waana Adamu karibu ya nyayo zake."

Wao wakasikia maneno yake wakamfungua wakamwacha aende zake, wakatafuta ngamia wao wakamkuta kuko huko mwituni wala hakwenda mbali, yuko karibu anakula majani tu

Wao wakarudi wakampeleka zawadi yule masikini, wakastaajabu kuona akili yake.

ADABU.

Mtu akiambiwa na mwenzake, "Huna adabu wee!", mtu huyu huona ametukanwa. Bassi ginsi gani watu wengi hawayafikiri sana mambo ya adabu ?

Huko Ulaya katika Waingereza watu husema, "Adabu ndizo rahisi, lakini vingi vinanunuliwa nazo." Maana watu wenyi adabu hupata kupendwa, hutendwa vema, sababu watu hupendezewa nao sababu ya adabu zao.

Tena watu wenyi adabu huheshimiwa. Mtu akikuondokea akikuheshimia, huna buddi kumheshimia mwenyewe kumkaribisha vizuri.

Akiwa mtu akikuambia, "Haya nipe kitu fullani!", akisema na ukali hatta unastuka kwa ginsi apalizavyo sauti yake ; akija tena mtu wa pili akingoja mpaka unakwisha utendavyo ama usemavyo, kiisha anasema na upole na taratibu, "Tafathali unipe kitu fullani," katika hawa wawili nani ndiye utakayempenda kupa atakacho ? Siye huyu mwenyi kutaka na upole ?

Bassi hii ndiyo maana vitu vinanunuliwa na adabu.

Labuda tena u aingia katika nyumba ya mtu; mwenyi nyumba atakuondokea, atakukaribisha vizuri, atakuweka mahali pazuri, atakusikiliza; labda hana nyumba kubwa, wala hana chakula kizuri cha kukuletea, lakini utapendezwa na adabu zake, utakuja tena kuongea naye, utamtaka kuwa rafiki yako.

Tena watu wathanio wajithili kwa ginsi wanamheshimu mwenzao, hukosa sana. Labuda utaingia chumbani; mle kuna watu wawili, mmoja wao anakuondokea, anakukaribisha anakuletea kiti chake; wa pili hukaa kitako anakutazama tu, wala haondoki, wala hasemi neno, anakukodolea macho tu. Bassi katika hao wawili utasema nani ndiye mngwana? nani ndiye mwenyi kufundishwa? Siye huyu wa kwanza?

Hatta sasa nimesifu adabu kwa uzuri wake, na fayida yake, lakini kwa watu Wamasihiya imewapasa kufikiri upole wake Isa Masiya Bwana wetu, na maneno ya Petro mtume akituambia, "Mwaheshimie wote."

MWISHO.



This book should be returned to the Library on or before the last date stamped below.

A fine is incurred by retaining it beyond the specified time.

Please return promptly.

3235107

MAR 16 1 H

CANCELLED